

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI**



TAARIFA KWA UMMA

MFUMO MPYA WA MALIPO SERIKALINI

Serikali inapenda kuwatangazia wananchi wote na umma kwa ujumla kuwa ipo katika mchakato wa kuanzisha utaratibu wa kufanya malipo moja kwa moja katika akaunti za walipwaji kwa kupitia mtandao wa malipo wa Benki Kuu ya Tanzania (Tanzania Interbank Settlement System – TISS) kuanzia mwezi Julai 2010.

Mfumo huo mpya wa malipo unahitaji makampuni na watu binafsi wanaofanya biashara na Serikali kwenye Wizara, Idara za Serikali na Mikoa kuwasilisha taarifa zao za benki na biashara ili ziweze kuingizwa katika mtandao wa malipo wa Serikali [Integrated Financial Management System (IFMS)]. Wahusika watatakiwa kujaza fomu maalum ambazo watazipata kwenye Wizara, Idara na mikoa wanakotoa huduma

Fomu hiyo itajazwa taarifa zifuatazo:

1. Namba ya Akaunti ya Benki
2. Namba ya Tawi la Benki

3. Jina la Akaunti
4. Aina ya Akaunti
5. Namba ya kuandikishwa biashara
6. Namba ya kuandikishwa kampuni
7. Namba ya Mlipa kodi
8. Jina la Benki na Jina la Tawi

Taarifa hizo zinahitajika kwa kuwa ni muhimu ili kuwezesha malipo kufanyika kwa mlipwaji.

- Aidha Mfumo huu mpya utafanywa kwa awamu mbili kama ifuatavyo: Awamu ya kwanza itazihusu Wizara na Idara za Serikali zilizopo Dar es Salaam ikiwa ni pamoja na Mkoa wa Dar es Salaam ambao pia malipo yake hulipwa kupitia Ofisi Kuu ya malipo iliyopo Wizara ya Fedha na Uchumi (Central Payment Office – CPO).
- Awamu ya pili itahusisha Wizara, Idara za Serikali na Mikoa yote ambayo malipo yake hayalipwi kupitia Ofisi Kuu ya malipo.

Ramadhani M. Khijjah
KATIBU MKUU WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI
26 Mei, 2010